



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BENKI KUU YA TANZANIA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. LD.170/515/02/1305

24 Juni 2026

Kwa:

Benki zote;

Taasisi za Fedha;

Waendeshaji wa Huduma za Fedha kwa Simu;

Watoaji wa Fedha za Kielektroniki ; na

Kampuni za Teknolojia za Fedha.

YAH: TANGAZO RASMI LA UFUNGUZI WA DIRISHA LA KUNDI LA TATU LA MAZINGIRA YA UDHIBITI WA MAJARIBIO YA TEKNOLOJIA YA FEDHA YA BENKI KUU YA TANZANIA

Benki Kuu ya Tanzania inapenda kutangaza rasmi ufunguzi wa dirisha la kupokea maombi ya ushiriki katika Kundi la Tatu la Mazingira ya Udhibiti wa Majaribio ya Teknolojia ya fedha ya Benki Kuu ya Tanzania. Kampuni za Teknolojia za Fedha na watoa huduma za fedha wenye nia ya kushiriki wanakaribishwa kuwasilisha maombi yao kupitia Mfumo wa Maombi wa Mazingira ya Udhibiti ya Teknolojia ya Fedha kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Kanuni za Udhibiti wa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha za Mwaka 2024.

2. Ili kutuma maombi, tafadhali tembelea <https://frsp.bot.go.tz/> na ujaze fomu ya maombi mtandaoni. Mwongozo wa kina pamoja na vigezo vya ushiriki vinapatikana katika tovuti ya Benki Kuu ya Tanzania. Dirisha la maombi la Kundi la Tatu kwa sasa limefunguliwa na litafungwa siku ya **Ijumaa, tarehe 31 Julai 2026.**

3. Bidhaa au huduma za fedha ambazo kwa sasa hazisimamiwi na mifumo iliyopo ya udhibiti wa Benki Kuu ya Tanzania pekee ndizo zitakazopokelewa kwa ajili ya kushiriki Mazingira ya Udhibiti ya Teknolojia ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania. Benki Kuu itakuwa na haki ya kuchapisha taarifa zozote muhimu za mwombaji katika tovuti yake, ikiwemo kwa madhumuni ya kubadilishana maarifa na kuimarisha ushirikiano na mamlaka nyingine za udhibiti za kimataifa, bila kufichua taarifa zozote zinazohusiana na haki miliki au mali za ubunifu za mwombaji.

4. Endapo kutakuwa na maswali au uhitaji wa ufafanuzi zaidi, tafadhali wasiliana na **Dkt. Sigsbert Rwiza** kupitia simu Na. **+255 713 998 593** au barua pepe Sigsbert.Rwiza@bot.go.tz, **Bw. Given Mhema** kupitia simu Na. **+255 711 788 830** au barua pepe Given.Mhema@bot.go.tz, na **Bw. January Bura** kupitia simu Na. **+255 685 474 952** au barua pepe January.Bura@bot.go.tz.



Sauda K. Msemu

Naibu Gavana

Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha